

TANGAZO LA SERIKALI Na. 121 la tarehe 25/4/2014
SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA) 1982

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA, 2012

**SEHEMU YA I
MASHARTI YA MWANZO**

Jina na tarehe ya 1. Sheria ndogo hizi zitaitwa za (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, 2012 na zitaanza kutumika mara baada ya kuchapwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

Sura ya 287 “Sheria” maana yake ni Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya ya mwaka 1982);

“Mwenyekiti”

(a) Linapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya.

(b) Linapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Kijiji maana yake ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji.

(c) Linapotumika kuhusiana na kamati, maana yake ni Mwenyekiti wa kamati;
“Kamati”

(a) Inapotumika kuhusiana na Halmashauri ya Kijiji ina maana ya Kamati iliyoanzishwa au iliyoteuliwa na Halmashauri ya Kijiji.

(b) Inapotumika kuhusiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata ina maana ya Kamati hiyo;

(c) Inapotumika kuhusiana na Kamati nyingine ina maana ya Kamati hiyo;

“Choo” maana yake ni chumba maalumu ambacho kimejengwa kwa ajili ya kuhifadhiya kinyesi au mkojo wa binadamu;

“Chombo cha takataka”, maana yake ni chombo cha kuwekea takataka kinachoweza kuhamishika, chenye mfuniko unaofunga vizuri, na mikono;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au mtu ye yote aliye tuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi.

“Hifadhi za wanyama” maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, vi umbe hai, na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na afisa mwidhiniwa chini ya sheria ndogo hizi au sheria nyingine ye yote.

“Kiwanda” maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa.

“Kuvuna misitu” maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kungo’ a miti au visiki.

“Maeneo ya hifadhi” maana yake ni pamoja na vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, mbuga za wanyama pori, maeneo ya mteremko na maeneo mengine yatakayotangazwa na Halmashauri kuwa maeneo ya hifadhi.

“Maeneo ya malisho” maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo aimetengwa na halmashauri.

“Maji” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji aliyoko chini ya ardhi na maji yaliyoko viwandani.

“Maji taka” kama ilivyo kaitka sheria ya mazingira 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani.

“Mazao ya misitu” maana yake kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya misitu na 14 ya Mwaka 2002 chini ya kifungu No. 2 ni kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana na misitu ni ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi utomvu maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai itakachotangazwa katika gazeti la serikali ni zao la msitu.

“Mazingira” kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya mazingira ya Mwaka 2004 maana yake itajumuisha vitu halisi vinavyomzunguka binadamu kama vile hewa, ardhi, maji hali ya hewa, sauti, mwanga, harufu, vionjo, viumbe visivyoonekana kwa macho hali ya kibaiolojia inayohusiana na wanyama, mimea, rasilimali za asili, masuala yote ya kijamii pamoja na mila na desturi, na inayojumuisha mazingira asilia na yale ya kutengenezwa na jinsi yanavyotegemeana.

“Mfugaji” maana yake ni mtu anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la halmashauri.

“Mifugo” maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu.

“Misitu” maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti inayoota upya ambayo inajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya sheria ya Misitu na 14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la halmashauri.

“Taka Ngumu” kama ilivyo katika sheria ya mazingira 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, inayotoa harufu mbaya, au kuhifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yeyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

“Taka ngumu” kama ilivyo katika sheria ya mazingira 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwanadani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughulia za uchumbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya maari mabovu (scraps).

“Eneo la Hifadhi” ni pamoja na maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji , hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

“Taka za Viwandani” kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya mazingira ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji Viwandani amba ni chanzo cha nishati, maji na mimea inayotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX.

“Uchafu hatari” kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya mazingira ya Mwaka 2004. Maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwanadani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athali za kikemia kwa binadamu au mazingira.

“Uchafu wa Mazingira” kama ilivyo katika sheria ya mazingira ya mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katiKa mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka amba unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama au ustawi, au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu katika sheria hii.

“Udongo” kama ilivyo katika sheria ya mzingira 2004 maana yake ni pamoja na dunia, machanga, miamba, miamba tope, madini uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi.

“Vitu hatari” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya mazingira 2004, ni kemikali yoyote, taka na gesi, madawa, vidonge, mimea na wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, masiaha au mazingira.

SEHEMU YA II **MASHARTI YA UFUGAJI**

Wajibu wa mfugaji 4.

Kila mfugaji chini ya sheria ndogo hizi:

- (a) Atatakiwa kufuga idadi ya mifugo itakayoamriwa na Halmashauri husika.
- (b) Atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri.

- (c) Atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo.
- (d) Atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri.
- (e) Atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri.
- Masharti kwa mfugaji 5 (1) Ni marufuku kwa mfugaji yeoyote:-
- (a) Kuchunga, Kulisha au mfugaji, kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;
- (b) Kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani.
- (c) Kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri.
- (d) Kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali.
- (e) Kuza au kununua mifugo katika maeneo mabayo siyo mnada, masoko au magilio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri.
- (f) Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri.
- Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo 6 (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ya mji au wilaya ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.
- (2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama itakavyoamriwa na Halmashauri husika.
- (3) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya muda uliopangwa na Halmashauri fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.
- (4) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda uliopangwa na Halmashauri, Halmashauri itarudisha fedha zake.

- | | | |
|---|--------|--|
| Ukaguzi
mifugo | wa 7 | <p>(1) Itakuwa halali kwa afisa kilimo na mifugo, maafisa watendaji wa kata na vijiji, afisa yejote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hii kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.</p> <p>(2) Mtu yejote atakaye wauzia maafisa waidhinishwa katika kifungu cha 7(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.</p> |
| Wajibu wa
halmashauri
kutenga maeneo ya
kulisha mifugo | 8 | <p>(1) Ni wajibu wa kila halmashauri kutenga maeneo maalum Halmashauri kutenga kwa ajili ya shughuli za kulisha malisho na kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri kwa mujibu wa sheria ya Ardhi sura 113 na Sheria ya Ardhi ya Kijiji sera ya 114 pamoja na sheria ya kuhifadhi mazingira.</p> <p>(2) Kila Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni, Minadani.</p> <p>(3) Ni marufuku kwa mfugaji yejote kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.</p> |
| Taratibu za ufugaji | 9. | <p>Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika sheria ndogo hii au sheria yejote iliyotungwa na Bunge la Jamahuri ya muungano wa Tanzania</p> |
| SEHEMU YA TATU
KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI | | |
| Taratibu za kilimo | 10 | <p>(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za Kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia sheria ya Ardhi sura 113 na 114 na sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge.</p> <p>(2) Itakuwa halali kwa Halmashauri kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa sheria ndogo itakayotungwa na Halmashauri.</p> |
| Masharti
mkulima | kwa 11 | <p>(1) Ni marufuku kwa mtu yejote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa afisa wa kilimo.</p> |

- (2) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa mtumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.
- (3) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto njia ya kuchoma isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa Halmashauri.
- (4) Kibali kitakachotolewa chini ya sheria hizi ndogo kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.
- (5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya sheria hizi ndogo ni kuanzia saa 12:00 Asubuhi hadi 4:00 Asubuhi.
- (6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko (crops rotation).
- Uhifadhi wa ardhi 12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanarudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda kiti au kutoendelea ku haribu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.
- Uchimbaji na 13. (1) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa, kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri.
- Ujenzi 14. (2) Uchimbaji wa madini uzingatie Sheria ya Madini pamoja na taratibu zilizowekwa na Halmashauri.
- Wajibu wa 15. (1) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kujenga nyumba au Holela jengo lolote katika eneo la hifadhi.
- Halmashauru na 16. (2) Kila Halamashauri itawajibika kusimamia kulinda na kusimamia vyanzo vya maji.
- kulinda vyanzo na (2) Kila mtu atawajibika kushiriki katika shughuli ya hifadhi ya vyanzo vya maji na mtu ye yeyote ambaye atashindwa bila sababu za msingi atachukuliwa hatua kali za sheria na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria Ndogo hizi.
- Kulinda eneo la na (1) Ni marufuku kwa mtu ye yeyote kulima, kukata miati, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote atachukuliwa hatua kali za kisheria na Halmashauri.

- Uchafuzi wa vyanzo vya maji 17 (2) Wajibu wa kila Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu itakuwa ni katika vyanzo vya maji.
- (3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa Halmashauri husika tu.
- Kuchoma au kusababisha moto 18 (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote, kiwanda, Taasisi, Shirika, Vyanzo vya kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, Ziwa, Visima, Mifereji, Chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji au viumbe vingine vilivyo hai.
- (2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.
- SEHEMU YA NNE: MISITU**
- Ukataji miti 19 (1) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchoma moto msitu kwa namna yoyote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri.
- (2) Iwapo moto uatatokea katika eneo la Halamashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa amri kwa wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhamana kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.
- (3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.
- (1) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyofadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.
- (2) Afisa misitu atatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.
- (3) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na afisa misitu kwa ajili ya kuchomea makaa huo.
- (4) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuvuna miti katika msitu ambaa umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambaa ni rasilimali kwa taifa.

- Wajibu wa
Kupanda miti
20. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

**SEHEMU YA TANO
TAKA NGUMU NA LAINI**

- Utupaji wa taka
ngumu na laini
- 21 (1) Taka zote katika eneo la Halmashauri zitatupwa katika eneo maalum au jalala kuu lililotengwa au litakalotengwa na Halmashauri kwa ajili hiyo na Halmashauri itawajibika kusimamia kwa usafi katika eneo lake.
- (2) Mtu yejote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au Kujisaidia katika kingo za bahari, mito, maziwa, Mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika eneo la Halmashauri yoyote atakuwa ametenda kosa na akithibitika kufanya kosa hilo ataadhidiwa chini ya Sheria Ndogo hizi.
- (3) Mtu yejote anawajibika kuwa na choo salama, na kwa misingi hiyo si ruhusa kwa mtu kukojoa, kunya au kumwaga mkojo, kinyesi au matapishi katika mtaa, eneo la jamii, uchochoroni, njiani, barabarani, sehemu yoyote au katika eneo lolote isipokuwa katika choo na kwa kuzingatia usafi wa choo hicho.
- Uendeshaji wa
viwanda
22. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makati ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

**SEHEMU YA SITA
MAKOSA NA ADHABU**

- Makosa
23. Mtu yejote ambaye:-
- (a) Ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
- (b) Atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali.
- (c) Atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;
- (d) Atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa.
- (f) Atakiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchang'a, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
- (g) Atakiuka masharti ya kuhifadhi ardhi
Atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji.
- (h) Atachoma au kushiriki katika kuanzisha moto au,
- (i) Hatashiriki katika shughuli ya kuzima moto bila ya sababu ya msingi;
- (j) Atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa au

- (k) isiyohifadhiwa bila kibali;
- (l) Atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;
- (l) Atafyeka nyasi, kung'oa vichaka, na kung'oa viski katika misitu bila kibali;
- (m) Atatupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa katika Sheria ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (n) Hana choo na atajisaidia haja kubwa au ndogo au atatupa uchafu wa aina hiyo mahali pasipostahili au mahali ambapo siyo chooni;
- (o) Atatiririsha maji machafu yanayoweza kuleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa amaeetenda kosa.
- (p) Ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbaa katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.
Na akipatikana na hatia atalipa faini ya isiyopungua shilingi elfu hamsini au isiyozidi shilingi laki mbili au adhabu ya kifungo cha miezi sita au adhabu zote mbili faini na kifungo au adhabu kama zilivyooneshwa katika sheria ya Mazingira, 2002.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mukutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 mwezi wa 10 Mwaka 2012 na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

Ibrahim Matovu
**MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA
MUHEZA**

Amir Abdulrahman Kiroboto

**MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA
MUHEZA**

Nakubali

Mhe. MIZENGO PETER PINDA
WAZIRI MKUU
DODOMA.